Habari Leo Uk 11, Mei 28, 2021

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI



Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki (Mb)
WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI



Mhe. Abdallah Hamis Ulega (Mb)
NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI



Prof. Elisante Ole Gabriel
KATIBU MKUU WA SEKTA YA MIFUGO



Dkt. Rashid Tamatamah
KATIBU MKUU WA SEKTA YA UVUVI

## MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2021/2022

Scanned with CamScanner

38. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2021, takriban tani **422,859.78** za samaki zenye thamani ya shilingi **trilioni 2.62** zilivunwa katika maji ya asili na jumla ya vifaranga vya samaki **20,040,000** vilizalishwa pamoja na tani **22,793.2** zilivunwa kupitia ukuzaji viumbe maji. Aidha, idadi ya mabwawa imeongezeka kutoka **27,979** hadi kufikia **30,032** na vizimba kutoka **431** mwaka 2019/2020 hadi **473**.

39. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2020/2021, jumla ya meli sita **(6)** zilipata leseni ya kuvua Ukanda wa Uchumi wa Bahari. Kati ya hizo, meli tatu **(3)** ni za kigeni na tatu **(3)** ni za wazawa. Meli hizo zimewezesha kuvuna jumla ya tani **437** za samaki.

## UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KATIKA MWAKA 2020/2021 NA MPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

### Kodi, Ada na Tozo katika Sekta ya Uvuvi

40. **Mheshimiwa Spika,** Serikali imepunguza viwango vya tozo na ada mbalimbali katika uzalishaji na usafirishaji wa mazao ya uvuvi nje ya nchi kupitia Kanuni iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 491A la tarehe 29 Juni, 2020 iliyoanza kutumika Julai 2020 ili kupunguza gharama na kuhimili ushindani wa kibiashara ndani na nje ya nchi. Baadhi ya viwango vya tozo vilivyopunguzwa na kuanza kutumika ni kama ifuatavyo:-

(i) Tozo ya usafirishaji wa dagaa nje ya nchi kutoka Ziwa Tanganyika imepungua kutoka Dola za Marekani **1.5** hadi Dola za Marekani **0.5** kwa kilo;

(ii) Tozo ya usafirishaji wa dagaa nje ya nchi kwa dagaa wa bahari, Ziwa Nyasa na Ziwa Victoria kutoka Dola za Marekani **1** hadi Dola za Marekani **0.16**;Ada ya leseni ya kusafirisha dagaa nje ya nchi kwa wafanyabiashara wadogo imepungua kutoka Dola za Marekani **1,000** hadi Dola za Marekani **250** na kwa Wafanyabiashara wakubwa kutoka Dola za Marekani **1,800** hadi Dola za Marekani **500**;

(iii) Ada ya leseni ya mazao mengine ya bahari kama Pweza, Kambakoche na Kaa imepungua kutoka Dola za Marekani **2,500** hadi Dola za Marekani **500** kwa Wafanyabiashara wadogo na kutoka Dola za Marekani **2,700** hadi Dola za Marekani **1,000** kwa Wafanyabiashara wakubwa; na

(iv) Tozo ya usafirishaji wa samaki aina ya migebuka kwenda nje ya nchi imepungua kutoka Dola za Marekani **0.5** hadi Dola za Marekani **0.3** kwa kilo.

### Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi

41. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2020/2021 kwa kuzingatia Mkakati Shirikishi wa Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi, Wizara imefanya ulinzi na usimamizi shirikishi katika Ziwa Victoria, Tanganyika, Nyasa na Bahari ya Hindi. Juhudi hizi zimewezesha kupungua kwa uvuvi haramu kwa asilimia **80** katika maji baridi na asilimia **100** katika matumizi ya vilipuzi baharini.

42. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati Shirikishi wa Usimamizi na Udhibiti wa Rasilimali za Uvuvi.

### Uboreshaji wa miundombinu ya mialo na masoko

3. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2020/2021 Serikali ilipanga kufanya ukarabati na ujenzi wa mialo na masoko. Hata hivyo, utekelezaji wake ulikabiliwa na changamoto ya kuwepo kwa mvua kubwa zilizonyesha katika msimu wa mwaka 2020 na hivyo kusababisha baadhi ya miundombinu kuharibika na mingine kufunikwa na maji, hususan katika mialo ya Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria. Hali hii imechelewesha utekelezaji wa kazi katika mialo ya Muyobozi (Uvinza), Kasanga (Kalambo) na Kirando (Nkasi) katika Ziwa Tanganyika na Kigangama (Magu), Ghana (Ukerewe), Nyamikoma (Busega) na Marehe (Bukoba) katika Ziwa Victoria ambako jumla ya Shilingi **589,068,327** zilitengwa.

44. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Majengo (TBA) inafanya ukarabati wa maeneo **9** kwa gharama ya Shilingi **1,490,931,673**. Maeneo hayo ni pamoja na mialo ya Ihale (Busega), New Igombe na Kayenze (Ilemela), Igabilo (Bukoba), Chifunfu/Kijiweni (Sengerema), soko la Mbamba-Bay (Nyasa) na Ofisi za Vituo vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi vya Busega, Sengerema na Sota.

45. **Mheshimiwa Spika,** kuhusu mauzo ya mazao ya uvuvi nje ya nchi, hadi kufikia Aprili 2021, jumla ya tani **32,962.79** za samaki na samaki hai wa mapambo **141,592** wenye thamani ya shilingi **Bilioni 335.25** ziliuzwa nje ya nchi na kulingizia Taifa mrabaha wa shilingi **Bilioni 15.55** ikilinganishwa na tani **35,329.36** na samaki hai wa mapambo **102,458** yenye thamani ya shilingi **Bilioni 436.96** yaliyouzwa nje ya nchi katika kipindi kama hiki mwaka 2019/2020.

46. **Mheshimiwa Spika,** Kiasi cha mazao ya uvuvi yaliyouzwa nje ya nchi kimepungua kwa asilimia **6.70** ikilinganishwa na kiasi kilichouzwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2019/2020. Kiasi cha mrabaha kilichokusanywa kutokana na mauzo hayo kimepungua kwa asilimia **25.27.** Hali hii imechangiwa na kuyumba kwa soko la mazao ya uvuvi nje ya nchi kutokana na mlipuko wa Homa Kali ya Mapafu (UVIKO 19). Vilevile, upungufu huo umesababishwa na kupungua kwa kiasi cha samaki kinachochakatwa viwandani ambacho ndicho kinachosafirishwa nje ya nchi. Aidha, upungufu wa malighafi viwandani, unachangiwa na kuibuka kwa biashara ya mabondo ambapo bondo pekee lina bei kubwa kuliko bei ya samaki mwenye bondo ndani yake. Kutokana na hali hiyo, wavuvi wanashawishika kutenganisha bondo na samaki ambapo bondo huuzwa kwenye viwanda vya kuchakata mabondo na samaki kwenye soko la ndani, na hivyo kupelekea kupungua kwa samaki wazima (whole fish) wanaouzwa kwenye viwanda vya kuchakata samaki.

### Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU)

47. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2020/2021 Serikali kupitia MPRU imeendelea kusimamia na kuratibu shughuli za uhifadhi katika bahari. Katika mwaka 2021/2022 MPRU kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii na Mamlaka nyingine za Serikali itaboresha mazingira ya uwekezaji wa utalii wa kiikolojia katika visiwa na fukwe.

### Usimamizi wa Uvuvi katika Bahari Kuu

48. **Mheshimiwa Spika,** Ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 23/02/2021 Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Sura 388 ya mwaka 2020 iliwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar na kuorodheshwa kulingana na masharti ya ibara ya 132 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 toleo la 2010. Hali hii itaiwezesha Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake.

49. **Mheshimiwa Spika,** Kanuni mpya za Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu zimetayarishwa, zimesainiwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 334 ya tarehe 23 Aprili, 2021. Kanuni hizi zitawezesha kutekeleza kikamilifu Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura 388 ya mwaka 2020 ambayo pamoja na mambo mengine imeweka mazingira bora ya uwekezaji kwenye uvuvi wa Bahari Kuu kwa kutoa vivutio kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, masharti nafuu ya leseni kwa wazawa ili kuongeza ushiriki wa Sekta binafsi katika Uchumi wa Buluu nchini.

### Ukuzaji Viumbe Maji

50. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Aprili 2021 jumla ya vifaranga vya samaki **20,040,000** vilizalishwa katika vituo **34** vya Serikali na Sekta Binafsi ikilinganishwa na vifaranga **14,531,487** vya samaki vilivyozalishwa mwaka wa fedha 2019/2020 sawa na ongezeko la asilimia **37.9** wakati mahitaji halisi ya vifaranga **42,454,522**. Aidha, tani **875** za chakula cha samaki zimezalishwa ikilinganishwa na tani **58.45** mwaka 2019/2020 na mahitaji ya chakula tani **9,552.27**.

51. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2020/2021 Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) imepandikiza samaki **101,500** katika malambo ya Kongogo (Dodoma), Mwanduigembe (Singida), Mwalusho (Simiyu), Mahiga (Mwanza), Igigwa (Tabora), Mpera (Shinyanga), Wanging'ombe (Njombe) na Kitanda (Ruvuma) ikilinganishwa na samaki **1,500** waliopandikizwa mwaka 2019/2020.

52. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2021/2022 Wizara itawezesha kutambua na kufanya upembuzi yakinifu kwa maeneo yanayofaa kwa ufugaji samaki kwenye vizimba (Strategic Environmental Impact Assessment) kwa lengo la kupunguza gharama za uwekezaji. Zoezi hili litaanza na kanda mbili **(2)** katika Ziwa Victoria.

53. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2021/2022 Wizara imepanga kuanzisha mashamba darasa **40** katika Halmashauri **40** nchini kwa kushirikiana na OR - TAMISEMI. Aidha, Wizara itaanza ujenzi wa vituo vipya viwili **(2)** vya ukuzaji viumbe maji katika Mikoa ya Mtwara na Dar es Salaam ili kuhamasisha ufugaji wa viumbe maji bahari katika ukanda wa pwani. Aidha, Wizara itaendelea na ukarabati na upanuzi wa vituo vitano **(5)** ili kuongeza uzalishaji wa vifaranga vya samaki na huduma za ugani.

### Huduma za Ugani wa Uvuvi

54. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu itaendelea kuimarisha Huduma za Ugani ili kuongeza tija na ufanisi katika Sekta ya Uvuvi kama ilivyoainishwa katika Aya 180 mpaka 187 katika kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

### Taasisi Zilizochini ya Sekta ya Uvuvi

55. **Mheshimiwa Spika,** taarifa zinazohusiana na taasisi za utafiti, mafunzo na ugani zimeainishwa katika hotuba yangu Aya 108 mpaka 207. Hata hivyo, kwa umuhimu wa kipekee nitazungumzia kwa kifupi juu ya

Scanned with CamScanner

Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO).

56. **Mheshimiwa Spika,** katika mchakato wa kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) Wizara imekamilisha Muundo wa Shirika na kuwasilishwa kwenye Mamlaka husika na inaendelea na ukarabati wa majengo ya ofisi ya utawala na karakana ya ukarabati wa zana za uvuvi.

57. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, chini ya ufadhili wa Serikali ya Japan, TAFICO inatarajia kuanza uzalishaji wa barafu (Ice plant) na uhifadhi wa samaki (Cold Storage facility) ambayo itatumika kwa ajili ya Shirika na wavuvi wadogo ili kuongeza thamani na kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi. Vilevile, Shirika litaanza uvuvi wa bahari kuu kwa kutumia meli ya kwanza ambayo inatarajiwa kuwasili mwezi Januari, 2022 ambayo pia imefadhiliwa na Serikali ya Japan.

**Mradi wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi** (SWIOFish)

58. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2020/2021 kazi mbalimbali zimetekelezwa kupitia Mradi wa SWIOFish ikijumuisha ujenzi wa Maabara ya Utafiti wa Uvuvi Dar es Salaam na ofisi tano **(5)** za Vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU) katika Wilaya tano (5) za Ukanda wa Bahari ya Hindi ambazo ni Mkinga, Pangani, Chalinze, Bagamoyo na Lindi Vijijini;

**Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi** (Agriculture and Fisheries Development Programme – **AFDP)**

59. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2021/2022 Serikali kupitia Programu ya AFDP imepata mkopo wenye masharti nafuu kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo (International Fund for Agriculture Development - IFAD) kwa ajili ya kununua meli nne (4) za kuvua katika Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu chini ya TAFICO.

**Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi**

60. Mheshimiwa Spika, ili kuchochea uwekezaji katika uvuvi wa Bahari Kuu, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali itaanza ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Mbegani Bagamoyo. Uwepo wa bandari utawezesha meli zinazovua Bahari Kuu kuja kushusha samaki na hivyo kuchochea fursa za uwekezaji ikiwemo kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi na mitambo ya kuzalisha barafu.

**MAENEO YA VIPAUMBELE KATIKA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2021/2022**

61. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2021/2022 Wizara imepanga kutekeleza vipaumbele vinavyoendana na kufungamanisha Uchumi wa Buluu (Blue Economy) na Uchumi Shindani wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Vipaumbele hivyo ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kujenga Bandari ya Uvuvi na kununua meli tatu za uvuvi kwenye Ukanda Uchumi wa Bahari Kuu;

(ii) Kuimarisha miundombinu ya mialo, masoko, vichanja vya kukaushia samaki na kusimika maghala ya ubaridi na mitambo ya barafu kwa ajili ya kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi kwa wavuvi wadogo kwa kukarabati;

(iii) Kuweka mazingira bora ya uwekezaji kwenye uvuvi wa Bahari Kuu kwa kuweka masharti nafuu ya leseni kwa wazawa;

(iv) Kuhamasisha ufugaji wa samaki kwa kuanzisha mashamba darasa katika halimashauri 40 kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI;

(v) Kuimarisha miundombinu ya uzalishaji wa vifaranga na chakula cha samaki kwa kushirikisha sekta binafsi;

(vi) Kuimarisha ulinzi na usimamizi shirikishi pamoja na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi nchini; na

(vii) Kuweka Mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya utambuzi wa maeneo ya mavuvi ili kuongeza tija kwa wavuvi wadogo na kukusanya taarifa na takwimu za wakuzaji viumbe maji.

**HITIMISHO**

**Shukrani**

62. **Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuhitimisha hotuba yangu, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara kufanikisha majukumu yake. Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka uliopita yametokana na ushirikiano na misaada ya kifedha na kiufundi kutoka kwa nchi wahisani, mashirika mbalimbali ya kitaifa na kimataifa, taasisi za fedha za kitaifa na kimataifa, taasisi za hiari zisizokuwa za kiserikali na mashirika ya kidini bila kusahau hamasa na ushiriki wa wananchi wakiongozwa na Waheshimiwa Wabunge na Madiwani.

63. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wa kikanda na kimataifa kwa lengo la kuongeza ufanisi. Baadhi ya wadau hao ni: Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Benki ya Dunia (WB), AU-IBAR, OIE, Ubalozi wa Japan, Ubalozi Uholanzi.

64. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee nimpongeze na kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,** kwa namna anavyoliongoza Taifa letu tangu alipokula kiapo tarehe 19 Machi, 2021 na anavyotusimamia katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Nina imani kuwa ndani ya uongozi wake Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022 – 2025/202 vitatekelezwa kikamilifu hususan katika sekta za mifugo na uvuvi.

65. **Mheshimiwa Spika,** pia nichukue nafasi hii kumpongeza **Mhe. Abdallah Hamis Ulega**, Mbunge wa Mkuranga kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi na nimshukuru kwa kunisaidia kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, nawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara, **Prof. Elisante Ole Gabriel** (Mifugo) na **Dkt. Rashid Adam Tamatamah** (Uvuvi) kwa kuwa kiungo muhimu kati yangu na watumishi na kuniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi. Pia, ninawashukuru na kuwapongeza kwa dhati Watumishi wote wa Wizara yangu kwa kazi nzuri wanazofanya.

66. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Maswa Magharibi ambao muda wote wameendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya Jimbo na kitaifa, nataka niwahakikishie kuwa nipo tayari kuendelea kuwatumikia kwa juhudi, bidii, maarifa na ujasiri mkubwa ili kuleta mabadiliko ya kimaendeleo katika Jimbo – na nchi kwa ujumla.

C. **MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

67. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022, Wizara inaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya jumla ya shilingi **169,194,996,810.00** Kati ya fedha hizo, shilingi **47,844,949,810** kwa ajili ya Sekta ya Mifugo na shilingi **121,350,047,000** kwa ajili ya Sekta ya Uvuvi. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:-

**Fungu 99: Sekta ya Mifugo**

68. Mheshimiwa Spika, Wizara inaomba kutumia jumla ya shilingi **47,844,949,810** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Mifugo. Kati ya fedha hizo, shilingi **30,973,208,810** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **16,871,741,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wake ni kama ifuatavyo:-

(i) **Fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 30,973,208,810**
- Mishahara shilingi **19,269,097,810**
- Matumizi Mengineyo (OC) shilingi **11,704,111,000**

(ii) **Fedha za Matumizi ya Maendeleo shilingi 16,871,741,000**
- Fedha za Ndani, shilingi **16,871,741,000**; na
- Fedha za Nje shilingi - **Hakuna.**

**Fungu 64: Sekta ya Uvuvi**

69. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/2022 Wizara inaomba jumla ya shilingi **121,350,047,000** kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Sekta ya Uvuvi. Kati ya fedha hizo, **shilingi 22,205,681,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **99,144,366,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:-

(i) **Fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi 22,205,681,000.**
- Mishahara ni Shilingi **11,575,270,000**; na
- Matumizi Mengineyo (OC) ni **Shilingi 10,630,411,000.00.**

(ii) **Fedha za Matumizi ya Maendeleo shilingi 99,144,366,000**
- Fedha za Ndani: shilingi **62,550,000,000**; na
- Fedha za Nje : shilingi **36,594,366,000**

70. **Mheshimiwa Spika,** naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara: www.mifugouvuvi.go.tz

71. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Scanned with CamScanner

# Ulaji wa 'kitimoto' huathiri ufanisi wa ARVs

**Na Hadija Baghasha, Korogwe**

ULAJI wa nyama za nguruwe maarufu kama 'kitimoto' inasababisha magonjwa karibu 17, ambapo kwa watumiaji wa dawa za kufubaza makali ya virusi vya UKIMWI 'ARV' zinashindwa kufanya kazi ipasavyo. Hali hiyo inatokana na kuwepo mkubwa wa asidi.

Akizungumza katika kongamano la afya lililokuwa na kauli mbiu 'Pima afya yako kabla hujaugua' Mkurugenzi wa Zahanati ya Manundu, Dkt Ali Mzige amesema walaji wa nyama ya nguruwe maarufu 'kitimoto' wana uwezekano wa kupata tatizo la kifafa linalotokana na tegu inayokimbilia kwenye ubongo.

"Nyama ya nguruwe siyo white meat,hilo wajue lakini nyama hii ina magonjwa karibu 17 na husababisha madhara makubwa kwenye mwili," amesema Dkt. Mzige na kuongeza kwamba ulaji wa mbogamboga unasaidia kuondoa sumu mwilini.

Dkt Mzige amesema magonjwa mengi kama kisukari,shinikizo la damu na saratani husababishwa na watu kutozingatia kanuni za chakula wanachokula.



Dkt Ali Mzige akionyesha bango lenye picha ya mtu aliyeathirika kutokana na kuvuta sigara. (Na Mpigapicha Wetu)

Ameshauri watu wapunguze nishati lishe za ziada (extra calories) matumizi ya sukari,mafuta yenye lehemu (cholesterol) na chumvi.

"Tutumie vyakula vya asilia vyenye lishe makapi-fibre,kula dona badala ya sembe nyeupe,mihogo, magimbi, viazi vitamu vikipikwa kwa kuchemshwa bila kukaangwa ni bora kuliko chips," amesema Dkt Mzige.

Aidha, ametoa tahadhari kwa akina mama wajawazito wanaopendelea kula chips mayai wakati wa mimba kwamba chakula hicho kitawapa uwezekano wa kupata kisukari cha mimba.

Pia ameshauri akina mama wanaotengeneza unga wa lishe kwa ajili ya watoto kwamba unga huo uliokuwa na aina nyingi za nafaka haufai kwa matumizi ya watoto.

Dkt Mzige ametambulisha kituo chake kipya cha Mshangai Preventive Medical Care Polyclinic, itakayokuwa na jopo la madaktari bingwa watatoa huduma zote za magonjwa yanayotokana na matatizo mbalimbali ikiwemo saratani.

Scanned with CamScanner

# Serikali yapunguza tozo, ada mazao ya uvuvi

**Na Magnus Mahenge, Dodoma**

*WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imefanya mapitio ya tozo mbalimbali ili kuzibadilisha kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na kuongeza mauzo ya mazao ya mifugo nje ya nchi.*

Akiwasilisha Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 bungeni jana, Waziri Mashimba Ndaki alisema wizara yake imeamua kuzipitia tozo na kodi hiyo kwa lengo la kuondoa malalamiko kwa wadau.

"Wizara imefanya mapitio hususan tozo ya asilimia moja ya thamani ya mzigo kwa nyama zinazouzwa nje ya nchi na ada ya ukaguzi wa mazao ya mifugo," alisema Ndaki.

Kutokana na hali hiyo, alisema wizara imefanya mapitio ya tozo hizo ili kuzibadilisha lengo likiwa ni kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na kuongeza mauzo ya mazao ya mifugo nje ya nchi.

Pia imefanya maboresho ambayo yatawasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango wakati akiwasilisha Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021/2022 baadaye bungeni hapo.

Kuhusu Machinjio ya Dodoma, alisema yanaendelea na shughuli za uchinjaji wa mifugo kwa soko la ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia Aprili 30, mwaka huu, alisema jumla ya ng'ombe 41,020 na mbuzi 23,004 walichinjwa.

Aidha, katika kipindi hicho, machinjio ilianzisha huduma ya kuchakata nyama kulingana na mahitaji ya wateja ambapo jumla ya kilo 18,943.6 za nyama ya ng'ombe zilichakatwa kwa ajili ya masoko maalumu ya ndani ikiwemo Kampuni ya Ujenzi wa SGR ya Yapi Merkez.

Kwa upande wa soko la nje, jumla ya mbuzi na kondoo 17,732 walichinjwa na kuzalisha jumla ya kilo 159,588 (tani 160) kwa ajili ya wateja mbalimbali waliosafirisha nyama kwenda nchi za Oman, Qatar na Vietnam zikiwa zimepozwa, zimegandishwa na zimenyonyolewa.

Alitaja mafanikio yaliyopatikana mwaka 2020/21 baada ya serikali kuchukua machinjio hayo ni kuongezeka kwa idadi ya ng'ombe wanaochinjwa kwa mwezi kwa soko la ndani kutoka wastani wa ng'ombe 1,950 hadi ng'ombe 4,050.

Scanned with CamScanner

The Guardian Pg. 2.




e in
M

reassure
country
organs
k to foil
d keep
long. In

position
Samia
tioning
ng the
fective
not the

police
crime,
n the

nians
never
n or
d.



Prime Minister Kassim Majaliwa has a word in the National Assembly in Dodoma city yesterday with (from-L) Livestock and Fisheries deputy minister Abdallah Ulega, Livestock and Fisheries minister Mashimba Ndaki, and Deputy Minister of State in the President's Office (Regional Administration and Local Governments) Dr Festo Dugange. Photo: PMO

Scanned with CamScanner

# Wafanyabiashara wasitisha kupeleka ng'ombe machinjioni

**Kibaha.** Wafanyabiashara wamesitisha huduma ya kupeleka ng'ombe machinjioni wakishinikiza kukutana na uongozi wa halmashauri ya Kibaha ili kuondoa changamoto zilizopo, ikiwamo muda wa kufikisha bidhaa hiyo machinjioni.

Wafanyabiashara hao walisema muda wa mwisho kufikisha ng'ombe machinjioni ni saa 12 jioni, lakini wakati mwingine wamekuwa wakishindwa kutimiza sharti hilo.



"Muda waliotuelekeza ni saa 12 jioni, tuwe tumeshafikisha ng'ombe hapa machinjioni, lakini kuna wakati tunachelewa kwa sababu mbalimbali, hivyo hali hiyo haiturdhishi," alisema mfanyabiashara Aidani Mchiwa.

Ofisa Mifugo wa Wilaya ya Kibaha, Dk Charles Marwa alisema walilazimika kuweka utaratibu wa kufikisha ng'ombe kabla ya saa 12 jioni kwa kufuata sheria zinavyoagiza.

(Sanjito Msafiri)

Scanned with CamScanner

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**HOTUBA YA WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI MHE. MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2021/2022**





Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki (Mb.)
Waziri wa Mifugo na Uvuvi





Mhe. Abdallah Hamis Ulega (Mb.)
Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi



Prof. Elisante Ole Gabriel
Katibu Mkuu wa Sekta ya Mifugo





Dkt. Rashid Tamatamah
Katibu Mkuu wa Sekta ya Uvuvi

Scanned with CamScanner

The Guardian Pg.1 May 28,2021

# House blames govt as output falls amid surge in fish stocks

By Songa wa Songa, Dodoma

EFFORTS to control illegal fishing led to more sustainable fish stocks in Tanzanian water bodies but productivity in the fisheries sector remained low, with MPs yesterday blaming underinvestment.

TURN TO Page2

Scanned with CamScanner

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2021/2022

*(Hotuba kamili inapatikana www.mifugouvuvi.go.tz)*

## A. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosimamia Kilimo, Mifugo na Maji iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99 – Mifugo na Fungu 64 – Uvuvi) Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

1. Mheshimiwa Spika, Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa namshukuru sana **Mhe. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kuendelea kushika wadhifa huu. Aidha, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, Rais aliyeiongoza nchi yetu kwa uhodari na umahiri mkubwa wakati wa uhai wake tangu alipoingia madarakani. Napenda kuchukua nafasi hii, kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, AMINA.

2. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza **Mhe. Samia Suluhu Hassan** kwa kuapishwa kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Watanzania wana matumaini makubwa na **Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan**. Aidha, napenda kumpongeza **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango** kwa kuteuliwa na kisha kuthibitishwa na Bunge lako tukufu kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

3. **Mheshimiwa Spika,** nichukue fursa hii pia, kumpongeza **Mhe. Dkt. Husein Ally Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kushika nafasi hiyo. Vile vile nampongeza **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa**, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

4. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kukupongeza wewe binafsi, kwa kuliongoza vizuri Bunge letu Tukufu kwa weledi na umahiri mkubwa. Wewe pamoja na Naibu Spika umewezesha Bunge la **12** kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyowekwa.

5. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake **Mhe. Dkt. Christine Ishengoma**, Mbunge wa Viti Maalum na Makamu wake **Mhe. Almasi A. Maige**, Mbunge wa Jimbo la Uyui kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kuwawakilisha wananchi katika Bunge lako Tukufu la 12.

6. Mheshimiwa Spika, naomba kwa mara nyingine tena niwapongeze na kuwashukuru wananchi wa Jimbo ninaloliwakilisha, yaani Jimbo la Maswa Magharibi, kwa kunichagua na kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili Tukufu.

### Masuala yaliyozingatiwa katika Mpango wa Bajeti ya mwaka 2021/2022

7. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022 Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi umeandaliwa kwa kuzingatia maelekezo yaliyomo kwenye Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2021/2022 uliozingatia maeneo ya vipaumbele vya Kitaifa kama yalivyo kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Malengo Endelevu ya Maendeleo (Sustainable Development Goals - SDGs); Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III) kwa kipindi cha 2021/2022 - 2025/2026 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 hadi 2025. Aidha, Mpango na Bajeti umezingatia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II).

### SEKTA YA MIFUGO (FUNGU 99) UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2020/2021 NA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2021 /2022

### Maeneo ya Kipaumbele katika Mwaka 2020/2021

8. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2020/2021 maeneo ya kipaumbele katika Mpango na Bajeti ya Wizara kupitia sekta ya mifugo (Fungu 99) yaliyozingatiwa ni pamoja na:-

(i) Kuboresha kosaafu ya mifugo ili kuongeza tija na uzalishaji;
(ii) Kuboresha biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi;
(iii) Kuwezesha upatikanaji endelevu wa maji, malisho na rasilimali za vyakula vya mifugo;
(iv) Kuimarisha afya ya mifugo;
(v) Kuimarisha huduma za utafiti wa mifugo, huduma za ugani na mafunzo kwa wafugaji na maafisa ugani; na
(vi) Kuboresha utekelezaji wa sera, sheria na kanuni katika sekta ya mifugo.

### Kazi Zilizotekelezwa

9. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2020/2021 idadi ya mifugo hapa nchini inakadiriwa kuongezeka ikilinganishwa na mwaka 2019/2020 ambapo idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka **milioni 33.4** hadi **milioni 33.9**, mbuzi kutoka **milioni 21.29** hadi **milioni 24.5** na kondoo kutoka **milioni 5.65** hadi **milioni 8.5**. Aidha, kuku wameongezeka kutoka **milioni 83.28** hadi **milioni 87.7** ikiwa kuku wa asili wameongezeka kutoka **milioni 38.77** hadi **milioni 40.36**, kuku wa kisasa wameongezeka kutoka **milioni 44.51** hadi **milioni 47.34** na nguruwe kutoka **milioni 2.14** hadi **milioni 3.2**. Aidha, Sekta ya Mifugo katika mwaka 2020 ilikua kwa asilimia **5.0** na kuchangia asilimia **7.1** katika Pato la Taifa ikilinganishwa na kukua kwa asilimia **5** na kuchangia asilimia **7.4** katika Pato la Taifa mwaka 2019.

10. **Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa maziwa umeongezeka kwa asilimia **3** kutoka lita **bilioni 3.01** mwaka 2019/2020 hadi kufikia lita **bilioni 3.1** mwaka 2020/2021. Aidha, usindikaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita **milioni 74.3** mwaka 2019/2020 hadi lita **milioni 75.9** mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia **2.2**. Ongezeko hili limetokana na viwanda kuongeza usindikaji ambapo sasa usindikaji umeongezeka kutoka asilimia 20 hadi asilimia 30 ya uwezo uliosimikwa (installed capacity).

11. **Mheshimiwa Spika,** uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kutoka tani **701,679.1** mwaka 2019/2020 hadi tani **738,166** mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia **5.2**. Pia, katika mwaka 2020/2021 uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai **bilioni 3.58** mwaka 2019/2020 hadi mayai **bilioni 4.5** mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia **26**.

12. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 vipande vya ngozi milioni **11.77** vyenye thamani ya shilingi **bilioni 25.93** vimezalishwa ikilinganishwa na vipande milioni **11.23** vyenye thamani ya shilingi **bilioni 22.8** vilivyozalishwa mwaka 2019/2020. Aidha, jumla ya Wakaguzi wa ngozi **60** kati ya **113** walioteuliwa wamejengewa uwezo. Pia, Wachunaji Ngozi **423** wamepatiwa mafunzo katika machinjio za Jiji la Dar es Salaam. Vilevile, visu maalum **131** vimetolewa kwa wachunaji ngozi katika Mikoa ya Kagera na Simiyu. Aidha, upatikanaji wa ngozi bora katika viwanda viwili vikubwa vinavyozalisha bidhaa za ngozi umeongezeka kutoka asilimia **30** hadi asilimia **80**.

13. **Mheshimiwa Spika;** katika mwaka 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya ngozi itaendelea kusimamia wingi na ubora wa ngozi.

14. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2020/2021 ili kuboresha mifugo hapa nchini Wizara imeendelea kukiboresha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) kwa kukipatia madume bora nane **(8)** ya mbegu na kufikia jumla ya madume **37**. Katika njia ya asili dume moja linaweza kupanda majike **25** kwa mwaka. Lakini kwa mpango wa uhimilishaji dume mmoja anaweza kuzalisha dozi za mbegu kwa ajili ya majike **150,000** kwa mwaka. Kwa muktadha huo, madume **8** yaliyonunuliwa katika mwaka 2020/2021 yataweza kuzalisha dozi za mbegu kwa ajili ya majike **milioni 1.2** kwa mwaka. Kwa ujumla wake madume **37** yanawea kuzalisha dozi za mbegu kwa ajili ya majike **milioni 5.6** kwa mwaka.

15. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kuimarisha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC), Vituo saba **(7)** vya Uhimilishaji vya kanda na kuwezesha uendelezaji na uanzishaji wa kambi za uhimilishaji kwa lengo la kuhimilisha ng'ombe zaidi ya **1,000,000** kwa mwaka pamoja na kuwajengea uwezo wahimilishaji **150** katika Halmashauri za Wilaya.

16. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2020/2021 jumla ya mitamba **18,012** ya maziwa na nyama kutoka katika mashamba ya Serikali na binafsi imezalishwa na kusambazwa kwa wafugaji ikilinganishwa jumla ya mitamba **16,809** iliyosambazwa

Scanned with CamScanner

mwaka 2019/2020.

17. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022 Wizara itanunua mitamba bora 300 ya ng'ombe wazazi aina ya Borani kwa ajili ya mashamba ya Serikali ili kuboresha uzalishaji wa mitamba katika mashamba hayo. Aidha, Wizara itasambaza kwa wafugaji mitamba **1,000** kwa bei ya ruzuku kutoka katika mashamba ya Serikali.

18. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2020/2021, jumla ya vifaranga vya kuku **milioni 88.3** vimezalishwa na kusambazwa nchini. Kati ya hivyo, vifaranga milioni **52** ni wa nyama, vifaranga milioni **29** ni vya kuku chotara na vifaranga milioni **7.4** ni wa kuku wa mayai ikilinganishwa na vifaranga milioni **70.3** vilivyozalishwa mwaka 2019/2020.

19. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kushirikiana na wazalishaji wa vifaranga vya kuku ili kuhakikisha wafugaji wanapata vifaranga bora katika ukuaji na ustahilivu wa magonjwa ili kujikomboa kiuchumi.

20. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/2021 hadi tarehe 30 Aprili, 2021 jumla ya ng'ombe milioni **1.8** mbuzi milioni **2.1** kondoo **360,745** na punda **191,656** wenye thamani ya shilingi Trilioni **1.5** waliuzwa katika minada hapa nchini ikilinganishwa na ng'ombe milioni **1.5**, mbuzi milioni **1.7**, kondoo **299,157** na punda **198,000** wenye thamani ya shilingi Trilioni **1.06** waliouzwa hapa nchini mwaka 2019/2020 kipindi kama hicho. Sababu za kuongezeka kwa biashara ya mifugo kwa soko la ndani imetokana na Serikali kutengeneza mazingira rafiki ya biashara ya mifugo na kutoa elimu juu ya taratibu na kanuni za biashara ya mifugo kwa wadau mbalimbali.

21. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kujenga na kukarabati minada ya mifugo ya upili na mipakani ili kuwezesha biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi pamoja na kuimarisha vituo vya doria vya kimkakati.

22. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2020/2021 Halmashauri za Wilaya kumi na saba **(17)** zimetenga jumla ya Hekta **271,661.11** kwa ajili ya malisho ya mifugo. Hivyo, maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho yameongezeka kufikia hekta **milioni 3.1** mwaka 2020/2021 ikilinganishwa na hekta **milioni 2.8** katika mwaka 2019/2020.

23. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa itaendelea kutenga maeneo kwa ajili ya malisho, kuimarisha miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo kwa kuchimba malambo na visima virefu hususan katika maeneo yenye uhitaji mkubwa wa maji.

24. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2020/2021 viwanda vya kutengeneza vyakula vya mifugo vimeongezeka na kufikia **154** kutoka viwanda **105** mwaka 2019/2020. Hivyo, kuongeza uzalishaji wa vyakula vya mifugo kutoka tani **900,000** mwaka 2019/2020 hadi tani **milioni 1.2** mwaka 2020/2021.

25. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji malisho na vyakula bora vya mifugo; kusimamia na kudhibiti ubora na usalama wa vyakula vya mifugo; kutoa mafunzo rejea kwa wakaguzi wa vyakula vya mifugo na maeneo ya malisho; na kuimarisha mashamba ya Serikali ya kuzalisha malisho na mbegu. Aidha, Wizara imeandaa mpango wa kuendeleza malisho aina ya Juncao katika Mashamba ya taasisi za Serikali, baadhi ya Halmashauri na Sekta binafsi kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 1,250.

26. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa mifugo inaendelea kutekeleza mikakati ya kudhibiti magonjwa ya mifugo yaenezwayo na wadudu. Katika mwaka 2020/2021 mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Jumla ya lita **15,579** ya dawa za kuogeshea mifugo zilisambazwa kwenye majosho **1,983** katika Halmashauri **162** zilizopo kwenye mikoa **25** Tanzania Bara.

(ii) Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 jumla ya michovyo **milioni 447** ya kuogesha mifugo imefanyika sawa na asilimia **110** ya lengo la kuogesha michovyo **milioni 405** ya mifugo.

27. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau iliendelea kutekeleza mikakati ya kudhibiti magonjwa ya mifugo ya mlipuko na yanayovuka mipaka. Katika mwaka 2020/2021 mafanikio yafuatayo yamepatikana:-

(i) Utoaji wa chanjo umefanyika kwa mbuzi na kondoo milioni **3.3** dhidi ya Ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi na Kondoo; ng'ombe milioni **5.5** dhidi ya Ugonjwa wa Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP); na ng'ombe milioni **2.5** dhidi ya Ugonjwa wa Miguu na Midomo.

(ii) Jumla ya dozi milioni **35.5** za Chanjo ya Matone ya Ugonjwa wa Mdondo (I,) zimezalishwa na kusambazwa katika mikoa yote. Aidha, jumla ya kuku milioni **57.8** walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa mdondo.

28. **Mheshimiwa Spika,** Ugonjwa wa Homa ya Nguruwe (African Swine Fever - ASF) ulilipuka kwa vipindi mbalimbali katika mwaka 2020/2021 na kusababisha jumla ya vifo **5,428** katika Halmashauri **18** Tanzania Bara. Ugonjwa huu hauna tiba wala chanjo hivyo nitoe wito kwa Halmashauri zote nchini kutoa elimu ya namna ya kujikinga na ugonjwa na pia pale kunapotokea mlipuko kutoa taarifa mapema kwa Wizara na kupulizia dawa ya kuuwa virusi ili kuzuia hasara inayoweza kuwapata wafugaji. Aidha, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu na wananchi kuwa Ugonjwa huo umedhibitiwa.

29. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa upatikanaji wa taarifa za magonjwa ya mifugo, kuwezesha uchanjaji wa wanyama milioni **25** dhidi ya magonjwa ya kipaumbele **13** yenye chanjo.

30. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa mafunzo rejea kwa Wafugaji katika Halmashauri **21** na pia kuwajengea uwezo (ToT) Maafisa Ugani kutoka katika Halmashauri za mikoa ya Dodoma na Singida **(20)**; Arusha, Kilimanjaro na Manyara **(21)** na Washauri wa Mifugo wa Mikoa yote Tanzania bara **(26)**. Aidha, idadi ya Mashamba Darasa ya malisho imeongezeka kutoka **88** mwaka 2019/2020 hadi **103** mwaka 2020/2021.

31. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kuwezesha utoaji wa huduma za ugani kwa kununua pikipiki **300** kwa ajili ya Maafisa Ugani, kuwezesha Halmashauri **20** kuanzisha mashamba darasa **60** ya malisho.

### Taasisi Zilizo Chini ya Sekta ya Mifugo

32. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo) inasimamia na kuratibu utendaji wa taasisi sita (6) ambazo ni; Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), Wakala ya Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA), Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI), Wakala ya Maabara ya Veterinari Tanzania (TVLA), Bodi ya Maziwa Tanzania na Bodi ya Nyama Tanzania.

33. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na umuhimu wa kukabiliana na changamoto ya uzalishaji wa ng'ombe na upatikanaji wa malisho. Nitazungumzia kwa ufupi Kampuni ya NARCO:-

(i) Kampuni ina eneo la malisho lenye ukubwa wa hekta **480,000** hivyo kuwa na uwezo wa kutunza unit za mifugo **240,000** kwa uwiano wa kitaalam wa hekta **2** kwa unit ya moja ya mifugo.

(ii) Kwa sasa kuna unit za mifugo **157,000** hivyo kuwa na eneo lililobakia lenye uwezo wa kutunza unit za mifugo **83,000** tu.

(iii) Asilimia **75** ya eneo la ranchi limekodishwa kwa wafugaji binafsi hivyo NARCO imebakiwa na asilimia 25 ya eneo kwa ajili ya mafunzo, utafiti na biashara za kampuni.

(iv) Baadhi ya ranchi za kampuni ya NARCO zina mifugo mingi zaidi ya uwezo wake hivyo watahamishiwa katika ranchi zingine. Mfano ranchi ya kongwa yenye ukubwa wa hekta **38,000** inatakiwa kutunza unit za mifugo wasiozidi **19,000** lakini kwa sasa kuna unit za mifugo **35,000**.

34. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya mapitio ya tozo zinazoathiri uwekezaji katika biashara ya mifugo lengo likiwa ni kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na kuongeza mauzo ya mazao ya mifugo nje ya nchi. Maboresho yaliyofanyika yatawasilishwa na Waziri wa Fedha na Mipango wakati akiwasilisha Muswada wa Sheria ya Fedha (Finance Bill) ya mwaka 2021/2022. Hatua, hiyo itawezesha viwanda vya ndani ikiwemo Tan Choice Ltd., Eliya Food Overseas limited, Chobo Investment, Alpha Choice, Machinjio ya Dodoma na wengine kuuza nyama nje ya nchi kwa ushindani.

35. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Wizara itaendelea kutathmini tozo na ada mbalimbali zitakazoonekana kuwa kero kwa wazalishaji na wafanyabiashara wa mifugo na mazao yake ili kuzifuta au kuzifanyia marekebisho.

36. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2021/2022, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (sekta ya mifugo) itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo;

(i) Kuboresha na kutafuta masoko ya mifugo na mazao yake ndani na nje ya nchi;
(ii) Kuboresha kosaafu za mifugo;
(iii) Kuboresha malisho, upatikanaji wa maji na vyakula vya mifugo;
(iv) Kuimarisha afya ya mifugo;
(v) Kuwezesha utafiti na mafunzo ya ugani; na
(vi) Kutekeleza mpango wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe na kopa mbuzi lipa mbuzi.

## SEKTA YA UVUVI (FUNGU 64)

### Hali ya Sekta ya Uvuvi

37. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Uvuvi ni miongoni mwa sekta muhimu ya uchumi inayochangia katika kuondoa umaskini na kukuza uchumi. Sekta hii imegawanyika katika tasnia za uvuvi kwenye maji asili na ukuzaji viumbe maji. Katika mwaka 2020, Sekta ya Uvuvi ilikuwa kwa asilimia **6.7** na kuchangia asilimia **1.7** katika Pato la Taifa. Sekta imeajiri wavuvi **195,435**, wakuzaji viumbe maji **30,064** na zaidi ya Watanzania **Milioni 4.5** kwenye mnyororo wa thamani. Vilevile, samaki huchangia takriban asilimia **30** ya protini inayotokana na wanyama.

Scanned with CamScanner

The Guardian pg.1 May 2021

# LIVESTOCK

Page 3

NARCO

PRODUCER OF KONGHA BEEF

Scanned with CamScanner

## From the National Assembly

Stories by NELLY MTEMA & KATARE MBASHIRU

# Robust master plan to revolutionise fishing sector

MINISTRY of Livestock and Fisheries is in final stages of implementing a robust 'Master Plan for Technical Assistance to Develop the Tanzania Fisheries sector, the National Assembly was told here yesterday.

The minister for Livestock and Fisheries, Mashimba Ndaki said the project was being implemented in collaboration with the Food and Agriculture Organisation (FAO).

He made the revelation when presenting budget estimates for his ministry, as he asked Members of Parliament to approve 169.2bn/- in recurrent and development expenditure for 2021/2022 financial year.

According to him, the Technical Assistance to Develop Tanzania Fisheries Master Plan aims at making a comprehensive review with a view to coming up with a new plan which will replace the current one which was drafted in 2002.

"Until now, several stages have been undertaken, among them, collecting baseline information to be used as crucial guidelines in preparation of the new plan," noted the minister.

He added that the final comprehensive draft of the plan is expected to be completed before the end of this financial year.

In the ministry's 2021/2022, the minister outlined nine key priority areas that the ministry plans to implement, among them, intensifying security and inclusive supervision as well as sustainable use of fisheries resources in the country.

Other priorities include sealing all loopholes for revenue loss on resources obtained from the fisheries sector, as well as strengthening revenue collection on fisheries products.

Mr Ndaki further told the august House that in the next financial year, his ministry plans to improve supervision of resources and investment on the sea economic zone, ensuring that there is supervision and control of the quality of fish produced in the country, as well as putting up proper infrastructure for fisheries and boosting fishing business in the country.

"We will also make sure that there is a good flow of information and proper statistics on fishing activities, strengthening research, veterinary education as well as other related matters," said Mr Ndaki.

The minister said other priorities will include increasing aquaculture projects to boost fish production, whereas the government plans in the next fiscal year to increase production and supply of quality fish seeds as a key factor to the expansion of fish farming in the country.

## FROM ZANZIBAR HOUSE OF REPRESENTATIVES

STORIES from MASATO MASATO

### Isles consumes 42,000 tonnes of fish annually, *House told*

ZANZIBAR consumes 42,000 tonnes of fish annually, against its capacity to produce 38,000 tonnes, experiencing a shortage of 4,000 tonnes, the House of

**Blue Economy and Fisheries Minister, Abdallah Hussein Kombo told the**

Scanned with CamScanner

The Guardian Pg.1 May 28,2021

# House blames govt as output falls amid surge in fish stocks

**By Songa wa Songa, Dodoma**

EFFORTS to control illegal fishing led to more sustainable fish stocks in Tanzanian water bodies but productivity in the fisheries sector remained low, with MPs yesterday blaming underinvestment.

**TURN TO Page2**

Scanned with CamScanner

.tz

HALIUZWI

MAJIRA UK 9, MEI 28, 2021




Scanned with CamScanner

# Uhaba wa nyama waikumba Kibaha

**Na John Gagarini, Kibaha**

WANANCHI wa Mji wa Kibaha wamekumbwa na ukosefu wa nyama ya ng'ombe baada ya wafanyabiashara wa kitoweo hicho kusitisha uchinjaji ng'ombe wakitaka kukutana na uongozi wa halmashauri hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari mmoja wa viongozi wa wauzaji nyama Kibaha, Aidan Mchiwa, alisema changamoto iliyojitokeza na kusababisha ng'ombe wasichinjwe ni kuzuiwa kuchinjwa kwa madai ya kucheleweshwa ng'ombe kufika kwenye machinjio ambayo yako chini ya Halmashauri ya Mji wa Kibaha.

Mchiwa alisema muda wa mwisho kufikisha ng'ombe kwenye machinjio ni saa 12:00 jioni siku moja kabla ya kuchinjwa kesho yake, lakini wakati mwingine wamekuwa wakishindwa kufika kwa muda huo kutokana changamoto mbalimbali hasa pale wanapochelewa kutoka mnadani.

"Inashangaza kuona wengine wakileta ng'ombe hata kwa kuchelewa wanaruhusiwa kuchinja huku wengine wakikataliwa kuchinja, jambo ambalo limesababisha wasichinje baada mwenzetu kukataliwa kuchinja akidaiwa kuchelewa kuleta ng'ombe machinjioni," alisema Mchiwa.

Alisema hali hiyo ilileta mtafaruku na kama ingeachwa bila kufanyiwa kazi, ingeendelea kujenga matabaka kwa baadhi ya wafanyabiashara wa ng'ombe.

Theresia Malongo alisema kitu kilichomshangaza ni pale ambapo alipochelewa kuwafikisha ng'ombe wake machinjioni na kukataliwa kupokelewa, lakini wakati huo mmoja wa wafanyabiashara alichelewesha kufikisha ng'ombe wake muda unaotakiwa, lakini alikubaliwa kuchinja.

Alisema hata hivyo siku iliyofuata alifikisha ng'ombe wake machinjioni muda unaostahili, lakini cha kushangaza daktari alichelewa kufika ambapo alifika saa 9:00 badala ya saa 7:00 usiku hivyo wengi wakakubaliana wasichinje kwa sababu hiyo.

Hata hivyo alisema aliwashawishi wenzake wachinje, lakini hafanikiwa hivyo akaamua kwenda kuchinja nje ya machinjio.

Alisema hatua hiyo ilisababisha uongozi wa halmashauri kuamuru nyama hizo kwenda kuteketezwa kwa kuwa taratibu hazikufutwa za kiafya.

Akitolea ufafanuzi huo, Ofisa Mifugo wa Wilaya ya Kibaha, Dk Charles Marwa, alisema walilazimika kuweka utaratibu wa kufikisha ng'ombe kabla ya 12:00 jioni kwa kufuata sheria zinavyoagiza.

Alisema hali hiyo ikiruhusiwa kuendelea, kuna uwezekano wa wafanyabiashara wasio waaminifu kuingiza ng'ombe wa wizi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha mkoani Pwani, Jenifa Omolo, alisema alipokea ombi la mfanyabiashara huyo kuchinja ng'ombe ingawa alichelewesha kufikisha muda unaotakiwa.

Alisema baada ya m,fanyabiashara huyo kueleza sababu za kushindwa kufika kwa wakati na kumuomba, alifanya hivyo baada ya kujiridhisha kuwa mjasiriamali huyo ni wa siku nyingi katika huduma hizo na hana tatizo.

Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Martin Ntemo, aliwataka wafanyabishara hao kuzingatia sheria ili kuendelea na shughuli zao, badala ya kufanya kazi kwa mazoea kwa kuwa nchi inaendeshwa kwa kufuata sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo.

Alitaka hatia zichukuliwe dhidi ya wote waliosababisha uwepo wa tofauti hiyo.

Kwa siku katika machinjio hayo wastani wa ng'ombe 40 wanachinjwa huku kila ng'ombe mmoja akilipiwa Sh 5,000 ikiwa ni tozo kwenda halmashauri.

HABARI LEO, MEI 27, 2021 UK. 20

Scanned with CamScanner

# Tanzania kuwa na kuku wa aina yake

NA MUSSA YUSUPH, *Dodoma*

NEEMA imewashukia wafugaji na wavuvi nchini, baada ya serikali kutangaza mpango wa kuongeza uzalishaji wa mifugo ukiwemo uzalishaji wa kuku maalumu wa asili wanatoka Tanzania pekee.

Katika mpango huo unaolenga kuiwezesha taifa kujitosheleza kwa kuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) inaendelea kufanya tafiti za uzalishaji wa kuku wa kienyeji aina ya 'horasi' kwa wafugaji nchini.

Akiwasilisha bungeni hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2021/2022 jana, Waziri wa wizara hiyo, Mashimba Ndaki, alisema idadi ya mifugo imeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2019/2020.

Alisema takwimu za Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi mwaka 2020, zilionyesha idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka milioni 33.4 hadi milioni 33.9, mbuzi kutoka milioni 21.29 hadi milioni 24.5 na kondoo kutoka milioni 5.65 hadi milioni 8.5.

Kadhalika, alisema, kuku wameongezeka kutoka milioni 83.28 hadi milioni 87.7 ambapo kuku wa asili wameongezeka kutoka milioni 38.77 hadi milioni 40.36, kuku wa kisasa wameongezeka kutoka milioni 44.51 hadi milioni 47.34 na nguruwe kutoka milioni 2.14 hadi milioni 3.2.

"Sekta ya mifugo katika mwaka 2020 ilikua kwa asilimia 5.0 na kuchangia asilimia 7.1 katika Pato la Taifa ikilinganishwa na kukua kwa asilimia tano na kuchangia asilimia 7.4 katika Pato la Taifa mwaka 2019.

"Uzalishaji wa maziwa umeongezeka kwa asilimia tatu kutoka lita bilioni 3.01 mwaka 2019/2020 hadi kufikia lita bilioni 3.1 mwaka 2020/2021, ambapo kati ya hizo, lita bilioni 2.17 zilitokana na ng'ombe wa asili na lita bilioni 0.93 zilitokana na ng'ombe wa kisasa," alieleza.

Waziri huyo alisema kati ya ng'ombe milioni 33.9 waliopo nchini, ng'ombe wa maziwa ni milioni 1.2 na kuwezesha usindikaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita milioni 74.3 mwaka 2019/2020 hadi lita milioni 75.9 mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 2.2.

Alifafanua kuwa ongezeko hilo limetokana na viwanda kuongeza usindikaji ambapo umeongezeka kutoka asilimia 20 hadi asilimia 30 ya uwezo uliosimikwa.

Mashimba alieleza kuwa hadi kufikia Aprili 30 mwaka huu, kulikuwa na viwanda vya kusindika maziwa 99 kati ya hivyo, viwanda 96 vinafanya kazi na viwanda vitatu havifanyi kazi kutokana na changamoto mbalimbali ukiwemo ushindani wa kibiashara.

"Uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kutoka tani 701,679.1 mwaka 2019/2020 hadi tani 738,166 kwa mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 5.2. Kati ya hizo, tani 508,355.17 ni za nyama ya ng'ombe, tani 102,137.22 za nyama ya mbuzi na kondoo tani 86,205.78 za nyama ya kuku huku tani 41,467.82 za nyama ya nguruwe," alibainisha.

### KUKU WA KIPEKEE TANZANIA

Katika mpango unaolenga kuliwezesha taifa kujitosheleza kwa kuku, alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia TALIRI, inaendelea kufanya utafiti wa uzalishaji wa kuku wa kienyeji aina ya horasi kwa wafugaji nchini.

Alibainisha kuwa mpango huo utaiwezesha nchi kuwa na aina yake ya kuku wa asili wazazi, kujitegemea katika uzalishaji wa kuku kwa kuwa na mashamba ya kuku wa asili wazazi.

Pia, alieleza utasaidia upatikanaji wa kuku wa asili mwenye uzito mkubwa kutoka gramu 500 hadi 750 kwa sasa hadi kufikia kilogramu 1.5 akiwa na umri wa miezi minne, kuongeza umbo na uzito wa yai la kuku wa asili kutoka gramu 25 hadi 45 ya sasa kufikia gramu 50 hadi 60.

Vilevile, alisema utaongeza kiwango cha utagaji wa mayai toka 40 hadi 60 ilivyo sasa hadi kufikia 150 hadi 200 kwa kuku kwa mwaka.

"Katika mwaka 2020/2021 uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai bilioni 3.58 mwaka 2019/2020 hadi mayai bilioni 4.5 mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia 26.

"Ongezeko hilo limesababishwa na kuongezeka kwa vituo vya kutotolesha vifaranga vya kuku kutoka 26 mwaka 2019/2020 hadi 28 mwaka 2020/2021 ambapo wananchi wamehamasika kufuga kuku ili kujikomboa kiuchumi," alieleza.

### BIASHARA YA NGOZI

Waziri Mashimba alisema hadi kufikia Aprili 30 mwaka huu, vipande vya ngozi milioni 11.77 (sawa na ng'ombe milioni 4.17, mbuzi milioni 5.96 na kondoo milioni 1.64) vyenye thamani ya sh. bilioni 25.9 vimezalishwa ikilinganishwa na vipande milioni 11.23 (sawa na ng'ombe milioni 4.03, mbuzi milioni 5.6 na kondoo milioni 1.6) vyenye thamani ya sh. bilioni 22.8 vilivyozalishwa mwaka 2019/2020.

Alisema katika kipindi hicho, vipande vya ngozi milioni 1.50 vyenye uzito wa kilo 7,951,004 (sawa na ng'ombe kilo 7,250,879, mbuzi, kondoo kilo 119,654 na punda kilo 580,480) vyenye thamani ya sh. bilioni 16.1 viliuzwa nje ya nchi.

Alizitaja nchi hizo kuwa ni Ghana, Nigeria, Italy, Ethiopia, Indonesia, Vietnam, Kenya na China ikilinganishwa na vipande vya ngozi vyenye uzito wa kilo 6,747,011 (sawa na ng'ombe 5,948,791, mbuzi, kondoo 114,904 na punda 683,317) vyenye thamani ya sh. bilioni 12.9 vilivyouzwa nje katika nchi za Ghana, China, Pakistan, Indonesia, Ethiopia, Nigeria na Italy mwaka 2019/2020.

Alibainisha kuwa sababu za kuongezeka kwa mauzo ya ngozi nje ya nchi ni kuongezeka kwa mahitaji ya ngozi katika nchi za Ghana na Nigeria.

### BIASHARA YA MIFUGO

Akizungumzia biashara ya mifugo, alisema mwaka 2020/2021 hadi Aprili 30 mwaka huu, ng'ombe 1,843,904, mbuzi 2,081,233, kondoo 360,745 na punda 191,656 wenye thamani ya sh. trilioni 1.5 waliuzwa katika minada mbalimbali.

Alisema sababu za kuongezeka kwa biashara ya mifugo imetokana na serikali kutengeneza mazingira rafiki ya biashara ya mifugo, kutoa elimu kuhusu taratibu na kanuni za biashara ya mifugo kwa wadau mbalimbali.

"Hadi Aprili 30, mwaka huu, sh. bilioni 12.2 zilikusanywa kutoka katika minada ya awali, upili na mpakani kama maduhuli ya serikali ikilinganishwa na sh. bilioni 7.9 zilizokusanywa kutoka katika minada ya awali, upili na mpakani mwaka 2019/2020 kwa kipindi kama hicho," alieleza.

### MAGONJWA YA MIFUGO

Waziri huyo wa Mifugo na Uvuvi, alisema katika mwaka 2020/2021, ng'ombe 1,036,769, mbuzi 680,906 na kondoo 192,906 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa Kimeta katika mikoa ya Arusha, Songwe, Manyara na Kilimanjaro.

Alisema jumla ya mitamba 162,843 imechanjwa dhidi ya ugonjwa wa kutupa mimba katika wilaya za Arusha, Karatu, Babati, Dodoma Mjini, Simanjiro, Iringa na Njombe.

Kadhalika, alisema matukio 210 ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa yalifuatiliwa na sampuli 610 zilichukuliwa ambapo mbwa 812,712 na paka 4,152 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa.

"Ugonjwa wa homa ya bonde la ufa umeendelea kufuatiliwa kwa kukagua na kuchukuwa sampuli kwa wanyama wote wanaotupa mimba kwa sababu ya uwepo wa mvua nyingi kwa mwaka huu. Napenda kulitaarifu Bunge kuwa nchi yetu bado iko salama," alieleza.

### SEKTA YA UVUVI

Kuhusu sekta ya uvuvi, alisema sekta hiyo imetoa ajira za moja kwa moja kwa wavuvi wapatao 195,435 na waliozaji vyombo vya 30,064 katika mwaka 2020/2021.

Aliongeza kuwa zaidi ya Watanzania milioni 4.5 wameendelea kupata mahitaji yao ya kila siku kutokana na shughuli mbalimbali za sekta hiyo zikiwemo kuunda na kutengeneza boti, kushona nyavu, biashara ya samaki na mazao yake.

Kulingana na taarifa za utafiti zilizofanyika katika Ziwa Victoria mwaka jana, alisema kiasi cha samaki katika ziwa hilo kimeongezeka kutoka tani 2,481,165 mwaka 2019 hadi tani 3,465,913 kwa ziwa zima, sawa na ongezeko la asilimia 29.27.

Alieleza kuwa ongezeko hilo limechangia kiasi cha samaki kilichopo katika maji yote kufikia tani 4,058,913.

"Shughuli za wavuvi wadogo huchangia asilimia 95 ya samaki wanaovuliwa nchini na asilimia tano iliyobaki huchangiwa na wavuvi wakubwa. Hadi kufikia Aprili mwaka huu, wavuvi wadogo wapatao 195,435 walishiriki moja kwa moja katika shughuli za uvuvi kwa kutumia vyombo vya uvuvi vipatavyo 58,231.

Aliongeza kuwa, "Wavuvi hao walivuna tani 422,859.78 za samaki zenye thamani ya sh. trilioni 2.62, kati ya hizo, tani 356,853.90 sawa na asilimia 84.39 ni kutoka maji baridi na tani 66,005.88 sawa na asilimia 15.61 ni kutoka maji chumvi," alieleza.

MAOMBI YA FEDHA

Waziri huyo alisema katika mwaka 2021/2022, aliiomba Bunge liidhinishe makadirio ya matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, sh. bilioni 169.1.

Alisema kati ya fedha hizo, sh. bilioni 47.8 kwa ajili ya sekta ya mifugo na sh. bilioni 121.3 kwa ajili ya sekta ya uvuvi.

## KONGAMANO



KATIBU wa NEC ya CCM, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Kanali Mstaafu Ngemela Lubinga (wa tatu kushoto), akishiriki Kongamano la Kidunia la Vyama vya Siasa vyenye Mrengo wa Kijamaa, lililoandaliwa Chama Cha Kikomunisti cha China kwa njia ya video, Ofisi Ndogo ya CCM ya Makao Makuu, Dar es Salaam, jana. Kutoka kushoto ni makatibu wasaidizi wa Chama, Mganwa Nzota, Emmanuela Kaganda na Jacqueline Liana. (Picha na Jumanne Gude).

# Wakandarasi watakiwa kuwafichua maofisa wa serikali wapenda rushwa

Na MWANDISHI WETU, *Dar es Salaam*

WIZARA ya Ujenzi na Uchukuzi, imewataka makandarasi kuwafichua maofisa wa serikali wanaowaomba rushwa wawape upendeleo katika zabuni za ujenzi ili hatua kali ziweze kuchukuliwa dhidi yao.

Agizo hilo lilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa wizara hiyo, Dk. Leonard Chamuriho, alipokuwa akifungua mkutano wa siku mbili wa mashauriano wa wadau wa sekta ya ujenzi ulioandaliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB).

Dk. Chamuriho, alisema mkandarasi anapopewa mradi kwa kutoa rushwa, mara nyingi miradi haikamiliki kwa wakati na wakati mwingine inafanywa kwa viwango vya chini hivyo kuisababishia serikali hasara kubwa kwa kuharibika kwa muda mfupi.

Pia, alisema sekta ya ujenzi ni eneo linalolalamikiwa kuwa uombaji wa rushwa hivyo unaofanya hivyo wafichuliwe mara moja.

"Sekta ya ujenzi ni eneo ambalo linalalamikiwa kwa rushwa hivyo ungeni mkono juhudi za serikali katika kupambana na vitendo vya rushwa kwa sababu kupata zabuni kwa rushwa hakukuendelezi bali kunakudidimiza," alisema Waziri Chamuriho.

Pia, alisema huu ni wakati mwafaka kwa makandarasi wazalendo kuungana na kutumia fursa zilizopo kutekeleza miradi mikubwa ya ujenzi kwa kuweka ubinafsi pembeni.

Aliongeza kuwa kazi nyingi za ujenzi zinafanywa na kampuni za nje kutokana na makandarasi wa ndani kukosa uwezo wa mitaji, mitambo ya kutosha na rasilimali watu hivyo kuungana ndiyo itakuwa suluhisho la matatizo yao.

"Serikali haifurahii kuona kandarasi kubwa kubwa zinafanywa na makampuni ya nje, acheni ubinafsi muungane mpate uwezo wa kuzifanya nyinyi kwasababu mkizifanya nyinyi gharama zitashuka na fedha zitabaki nchini," alisisitiza.

Hivyo, aliahidi kutoa tamko kuhusu utaratibu unaotumiwa na serikali kufanyakazi za ujenzi bila kutumia makandarasi maarufu kama Force Account, ambao umelalamikiwa na makandarasi.

Alisema serikali itatoa tamko hilo mwezi Juni kwenye mkutano wa mashauriano baina ya Bodi yaUsajili wa Makandarasi (CRB) na wadau wa sekta ya ujenzi unaotarajiwa kufanyika mkoani Mwanza mwezi Juni.

"Serikali inalifanyia kazi hilo na hata Mwenyekiti wa Bodi ya CRB amelizungumza hapa muwe wavumilivu tutalitolea tamko mwezi Juni mwaka huu kwenye mkutano wanne utakaofanyika mkoani Mwanza," alisema Waziri Chamuriho.

Waziri aliyasema hayo baada ya Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Wakandarasi, Mhandisi Consolatha Ngimbwa kumweleza kuwa utaratibu huo umesababisha maumivu makubwa kwa makandarasi wa ndani kwani kwa muda mrefu hawana kazi.

Alimweleza Waziri kuwa mwaka 2018 serikali iliamua kutumia utaratibu huo ikisema kuwa makandarasi wa ndani wamekuwa wakitoza fedha nyingi ambazo haziendani na miradi husika hivyo kulazimika kutekeleza miradi yake yenyewe ili kuokoa fedha nyingi.

Mhandisi Ngimbwa alisema wakandarasi wameshajifunza na wako tayari kuanyakazi kwa bei ya chini na kwa ubora wa hali ya juu kwani wameshapewa mafunzo ya mara kwa mara na bodi ya CRB na kwa sasa wameiva kufanya kazi hizo.

"Baada ya serikali kuanza utaratibu wa force account kwa maelezo kuwa bei za wakandarasi wa ndani ni kubwa tuliwapa mafunzo ya mara kwa mara

kuhusu namna ya kujaza zabuni, tulienda mikoa mbalimbali na kwa kweli wameiva na wako tayari kufanya kazi za serikali," alisema.

Scanned with CamScanner

# MUHTASARI WA HOTUBA YA WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI MHESHIMIWA MASHIMBA MASHAURI NDAKI (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2021/2022

*(Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya wizara: www.mifugouvuvi.go.tz)*

**A. UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayosimamia Kilimo, Mifugo na Maji iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Fungu 99 – Mifugo na Fungu 64 – Uvuvi) Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

2. ***Mheshimiwa Spika***, Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa namshukuru sana **Mhe. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini kuendelea kushika wadhifa huu. Aidha, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ilipokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, Rais aliyeongoza nchi yetu kwa uhodari na umahiri mkubwa wakati wa uhai wake tangu alipoingia madarakani. Napenda kuchukua nafasi hii, kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, AMINA.

3. ***Mheshimiwa Spika***, napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza **Mhe. Samia Suluhu Hassan** kwa kuapishwa kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Watanzania wana matumaini makubwa na **Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan**. Aidha, napenda kumpongeza **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango** kwa kuteuliwa na kisha kuthibitishwa na Bunge lako tukufu kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

4. ***Mheshimiwa Spika***, nichukue fursa hii pia, kumpongeza **Mhe. Dkt. Husein Ally Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kushika nafasi hiyo. Vile vile nampongeza **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa**, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

5. ***Mheshimiwa Spika***, napenda pia kukupongeza wewe binafsi, kwa kuongoza vizuri Bunge letu Tukufu kwa weledi na umahiri mkubwa. Wewe pamoja na Naibu Spika umewezesha Bunge la 12 kutekeleza majukumu yake kikamilifu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyowekwa.

6. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake **Mhe. Dkt. Christine Ishengoma**, Mbunge wa Viti Maalum na Makamu wake **Mhe. Almasi A. Maige**, Mbunge wa Jimbo la Uyui kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2020/2021 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa kuwawakilisha wananchi katika Bunge lako Tukufu la 12.

7. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kwa mara nyingine tena niwapongeze na kuwashukuru wananchi wa Jimbo ninaloliwakilisha, yaani jimbo la Maswa Magharibi, kwa kunichagua na kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwatumikia katika Bunge hili Tukufu.

**Masuala yaliyozingatiwa katika Mpango wa Bajeti ya mwaka 2021/2022**

8. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022 Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi umeandaliwa kwa kuzingatia maelekezo yaliyomo kwenye Mwongozo wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2021/2022 uliozingatia maeneo ya vipaumbele vya Kitaifa kama yalivyo kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Malengo Endelevu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals - SDGs*); Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III) kwa kipindi cha 2021/2022 – 2025/2026 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 hadi 2025. Aidha, Mpango na Bajeti umezingatia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II).

**SEKTA YA MIFUGO (FUNGU 99)**
**UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2020/2021 NA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2021 /2022**
**Maeneo ya Kipaumbele katika Mwaka 2020/2021**

9. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 maeneo ya kipaumbele katika Mpango na Bajeti ya Wizara kupitia sekta ya mifugo (Fungu 99) yaliyozingatiwa ni pamoja na:-

(i) Kuboresha kosaafu ya mifugo ili kuongeza tija na uzalishaji;
(ii) Kuboresha biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi;
(iii) Kuwezesha upatikanaji endelevu wa maji, malisho na rasilimali za vyakula vya mifugo;
(iv) Kuimarisha afya ya mifugo;
(v) Kuimarisha huduma za ugani wa mifugo, huduma za ugani na mafunzo kwa wafugaji na maafisa ugani; na
(vi) Kuboresha utekelezaji wa sera, sheria na kanuni katika sekta ya mifugo.

**Kazi Zilizotekelezwa**

10. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2020/2021 idadi ya mifugo hapa nchini inakadiriwa kuongezeka ya ikilinganishwa na mwaka 2019/2020 ambapo idadi ya ng'ombe imeongezeka kutoka **milioni 33.4** hadi **milioni 33.9**, mbuzi kutoka **milioni 21.29** hadi **milioni 24.5** na kondoo kutoka **milioni 5.65** hadi **milioni 8.5**. Aidha, kuku wameongezeka kutoka **milioni 83.28** hadi **milioni 87.7** ikiwa kuku wa asili wameongezeka kutoka **milioni 38.77** hadi **milioni 40.36**, kuku wa kisasa wameongezeka kutoka **milioni 44.51** hadi **milioni 47.34** na nguruwe kutoka **milioni 2.14** hadi **milioni 3.2**. Aidha, Sekta ya Mifugo katika mwaka 2020 ilikua kwa asilimia **5.0** na kuchangia asilimia **7.1** katika Pato la Taifa ikilinganishwa na kukua kwa asilimia **5** na kuchangia asilimia **7.4** katika Pato la Taifa mwaka 2019.

11. ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa maziwa umeongezeka kwa asilimia **3** kutoka lita **bilioni 3.01** mwaka 2019/2020 hadi kufikia lita **bilioni 3.1** mwaka 2020/2021. Aidha, usindikaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita **milioni 74.3** mwaka 2019/2020 hadi lita **milioni 75.9** mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia **2.2**. Ongezeko hili limetokana na viwanda kuongeza usindikaji ambapo sasa usindikaji umeongezeka kutoka asilimia 20 hadi asilimia 30 ya uwezo uliosimikwa (*installed capacity*).

12. ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kutoka tani **701,679.1** mwaka 2019/2020 hadi tani **738,166** mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia **5.2**. Pia, katika mwaka 2020/2021 uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai **bilioni 3.58** mwaka 2019/2020 hadi mayai **bilioni 4.5** mwaka 2020/2021 sawa na ongezeko la asilimia **26**.

13. ***Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 vipande vya ngozi milioni **11.77** vyenye thamani ya shilingi **bilioni 25.93** vimezalishwa ikilinganishwa na vipande milioni **11.23** vyenye thamani ya shilingi **bilioni 22.8** vilivyozalishwa mwaka 2019/2020. Aidha, jumla ya Wakaguzi wa ngozi **60** kati ya **113** walioteuliwa wamejengewa uwezo. Pia, Wachunaji Ngozi **423** wamepatiwa mafunzo katika machinjio za Jiji la Dar es Salaam. Vilevile, visu maalum **131** vimetolewa kwa wachunaji ngozi katika Mikoa ya Kagera na Simiyu. Aidha, upatikanaji wa ngozi bora katika viwanda vikubwa na vidogo vinavyozalisha bidhaa za ngozi umeongezeka kutoka asilimia **30** hadi asilimia **60**.

14. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa tasnia ya ngozi itaendelea kusimamia wingi na ubora wa ngozi.

15. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/2021 ili kuboresha mifugo hapa nchini Wizara imeendelea kukiboresha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) kwa kukipatia madume bora nane (8) ya mbegu na kufikia jumla ya madume 37. Katika njia ya asili dume moja linaweza kupanda majike **25** kwa mwaka. Lakini kwa mpango wa uhimilishaji dume mmoja anaweza kuzalisha dozi za mbegu kwa ajili ya majike **150,000** kwa mwaka. Kwa muktadha huo, madume **8** yaliyonunuliwa katika mwaka 2020/2021 yataweza kuzalisha dozi za mbegu kwa ajili ya majike **milioni 1.2** kwa mwaka. Kwa ujumla wake madume 37 yanaweza kuzalisha dozi za mbegu kwa ajili ya majike milioni **5.6** kwa mwaka.

16. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kuimarisha Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC), Vituo saba (7) vya Uhimilishaji vya kanda na kuwezesha uendelezaji na uanzishaji wa kanda za uhimilishaji kwa lengo la kuhimilisha ng'ombe zaidi ya **1,000,000** kwa mwaka pamoja na kuwajengea uwezo wahimilishaji **150** katika Halmashauri za Wilaya.

17. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 jumla ya mitamba **18,012** ya maziwa na nyama imezalishwa katika mashamba ya Serikali na binafsi na kusambazwa kwa wafugaji ikilinganishwa na jumla ya mitamba **16,809** iliyosambazwa mwaka 2019/2020.

18. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022 Wizara itanunua mitamba bora **300** ya ng'ombe wazazi aina ya Borani kwa ajili ya mashamba ya Serikali ili kuboresha uzalishaji wa mitamba katika mashamba hayo. Aidha, Wizara itasambaza kwa wafugaji mitamba **1,000** kwa bei ya nafuu kutoka katika mashamba ya Serikali.

19. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021, jumla ya vifaranga vya kuku milioni **88.3** vimezalishwa na kusambazwa nchini. Kati ya hivyo, vifaranga milioni **52** ni wa nyama, vifaranga milioni **29** ni vya kuku chotara na vifaranga milioni **7.4** ni wa kuku wa mayai ikilinganishwa na vifaranga milioni **70.3** vilivyozalishwa mwaka 2019/2020.

20. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kushirikiana na wazalishaji wa vifaranga vya kuku ili kuhakikisha wafugaji wanapata vifaranga bora katika ukuaji na ustahilivu wa magonjwa ili kuifanya kiuchumi.

21. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 hadi tarehe 30 Aprili, 2021 jumla ya ng'ombe milioni **1.8** mbuzi milioni **2.1** kondoo **360,745** na punda **191,856** wenye thamani ya shilingi Trilioni **1.5** waliuzwa katika minada hapa nchini ikilinganishwa na ng'ombe milioni **1.5**, mbuzi milioni **1.7**, kondoo **299,157** na punda **190,000** wenye thamani ya shilingi Trilioni **1.06** waliouzwa hapa nchini mwaka 2019/2020 kipindi kama hicho. Sababu za kuongezeka kwa biashara ya mifugo kwa soko la ndani imetokana na Serikali kutengeneza mazingira rafiki ya biashara ya mifugo na kutoa elimu juu ya taratibu na kanuni za biashara ya mifugo kwa wadau mbalimbali.

22. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022 Wizara itaendelea kujenga na kukarabati minada ya mifugo ya upili na mipakani ili kuwezesha biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi pamoja na kuimarisha vituo vya doria vya kimkakati.

23. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 Halmashauri za Wilaya kumi na saba (17) zimetenga jumla ya Hekta **271,661.11** kwa ajili ya malisho ya mifugo. Hivyo, maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho yameongezeka kufikia hekta **milioni 3.1** mwaka 2020/2021 ikilinganishwa na hekta **milioni 2.8** katika mwaka 2019/2020.

24. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa itaendelea kutenga maeneo kwa ajili ya malisho, kuimarisha miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo kwa kuchimba malambo na visima virefu hususan katika maeneo yenye uhitaji mkubwa wa maji.

25. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2020/2021 viwanda vya kutengeneza vyakula vya mifugo vimeongezeka na kufikia **154** kutoka viwanda **105** mwaka 2019/2020. Hivyo, kuongeza uzalishaji wa vyakula vya mifugo kutoka tani **900,000** mwaka 2019/2020 hadi tani **milioni 1.2** mwaka 2020/2021.

26. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji malisho na vyakula bora vya mifugo; kusimamia na kudhibiti ubora na usalama wa vyakula vya mifugo; kutoa mafunzo rejea kwa wakaguzi wa vyakula vya mifugo na maeneo ya malisho; na kuimarisha mashamba ya Serikali ya kuzalisha malisho na mbegu. Aidha, Wizara imeandaa mpango wa kuendeleza malisho aina ya Juncao katika Mashamba ya taasisi za Serikali, baadhi ya Halmashauri na Sekta binafsi kwenye

*Inaendelea Uk III*

Scanned with CamScanner

MJADALA

# Ndugai ashangaa sheria ilivyopita

Habel Chidawali, Mwananchi
hchidawali@mwananchi.co.tz

**Dodoma.** Spika wa Bunge, Job Ndugai amesema sheria ya utaifishaji mifugo inayoingia kwenye hifadhi ni mbaya, akahoji huenda ilipitishwa wakati wabunge wakiwa wamelala.

Spika Ndugai alitoa kauli hiyo jana bungeni na kuongeza kuwa kama wabunge hawakuwa wamelala, huenda yeye (Ndugai) alikuwa safarini, kwani haiwezekani kuwa na sheria ya namna hiyo.

Mchakato wa utungwaji wa sheria huanzia bungeni na baada ya kupitishwa na Rais kusaini ndipo inapokuwa sheria tayari kwa utekelezaji.

Kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wafugaji kuhusu Sheria namba 19 ya mwaka 2009 ambayo imetajwa wakati wote kuwa inawafilisi wafugaji.

"Mheshimiwa Waziri, moja ya mambo ya kutazama ni pamoja na sheria hii, haifai kwani mifugo inachungwa na watoto wadogo ambao hawajui mipaka ya ranchi iko wapi, sasa wakiingia kazi ni kutaifisha, siyo vizuri," alisema Ndugai.

Ndugai ambaye ni mbunge wa Kongwa alihoji kama sheria ni hivyo, inakuwaje tembo wanaoingia kwenye mashamba ya watu mbona wao hawataifishwi.

Katika hatua nyingine, Spika Ndugai alisema hakuna namna yoyote ya kufanya miujiza ili ranchi za Taifa ziwe na faida, badala yake akaitaka Serikali iachie sekta binafsi kazi hiyo.

**TAARIFA ZAIDI**

**Naye Mbunge wa Bukoba Vijijini, Jason Rweikiza alisema kwa tafsiri nyepesi ni kuwa Narco imeshindwa na haiwezi kusimama, hivyo wapewe wawekezaji binafsi.**

**14**

**Jumla ya ranchi zilizopo nchini ambazo ukubwa wake ni hekta 544,207.**

Ndugai alisema ranchi zilizo chini ya kampuni ya ranchi za Taifa (Narco) hazina uwezo na kuitaka Serikali kuachana na mpango huo kwa kuwa si jukumu lake kuchunga mifugo.

Tanzania ina ranchi 14 nchini ambazo zina ukubwa wa hekta 544,207, ambazo zilianzishwa kwa sheria ya makampuni ya mwaka 1968.

"Mimi nimezaliwa Kongwa pembezoni kwa Narco, hakuna kitu hata mifugo. Hivi waheshimiwa mkipita pale huwa mnaona ng'ombe, hamna walishakwisha wote," alisema Ndugai.

Alisema kumuweka Paul Kimiti kuwa mwenyekiti wa bodi ya Narco ni kutaka azeeke vibaya, badala yake wampe bodi nyingine.

Ndugai alisema pia uwekezaji wa kisingizio cha kuwapa vitalu wafugaji hakina mantiki, kwa kuwa wafugaji wanapewa vitalu kwa msimu wa mwaka mmoja tena katika eneo lisilokuwa na hati, jambo ambalo alilitaja kama ni kuwapotezea malengo wafugaji. Kauli ya Spika iliungwa mkono na Kamati ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo ambayo ilisema uwezo wa kuhifadhi mifugo kwa Narco ni kati ya ng'ombe 80,000 hadi 90,000, lakini waliopo ni 12,681 pekee (2019/20).

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk Christina Ishengoma alisema kiasi kidogo cha fedha zinazotengwa katika kamati hiyo zinasababisha kukosekana kwa mazingira bora na yenye tija katika shughuli za biashara ya mifugo.

Dk Ishengoma alisema kwa mwaka wa fedha 2020/21, wizara ilitengewa Sh16.9 bilioni ambazo ni kiasi kidogo ukilinganisha na umuhimu wa sekta hiyo.

Mbunge wa Nkasi Kaskazini, Aida Khenani alisema sheria mbovu na kanuni za uvuvi za mwaka 2019 zimekuwa mwiba mkali kwa wavuvi nchini.

Khenani alizungumzia uchomaji wa nyavu za wavuvi unafanywa bila kufikiria, kwani Serikali imeshindwa kuwakamata watengenezaji na wasambazaji.

"Maji ya maziwa na bahari yamegeuka kuwa laana badala ya baraka, wavuvi wananyanyaswa wakati zana kama hizo majirani zetu wanazitumia. Kwa nini watendaji wenu wanatumia nguvu zaidi?" alihoji Khenani.

Wabunge wengine waliochangia ni Kilumbe Ng'enda aliyesema zana duni na kanuni mbovu zinachangia kuua sekta ya uvuvi.

Ng'enda alieleza masikitiko yake kuhusu urasimu wa upatikanaji wa kibali cha uvuvi akisema bora mtu anayeomba kibali cha kwenda peponi kuliko anayetaka cha uvuvi.



Spika wa Bunge, Job Ndugai akizungumza bungeni alipokuwa akiongoza kikao cha 38 cha mkutano wa Bunge la Bajeti, jijini Dodoma jana. **Picha na Edwin Mjwahuzi**

**Sahihisho**

**Jana katika gazeti hili Uk. 24 tulikosea jina la Rais wa Zanzibar, Dk Hussein Mwinyi. Tunamuomba radhi kwa usumbufu wowote ulliojitokeza.**
**Mhariri**

# Wizara yawapa nafuu ya tozo wafugaji nchini

Sharon Sauwa, Mwananchi
ssauwa@mwananchi.co.tz

**Dodoma.** Wizara ya Mifugo na Uvuvi imerudisha tabasamu kwa wadau wa sekta ya mifugo baada ya kubadilisha tozo zilizokuwa zikilalamikiwa, ikiwemo tozo ya asilimia moja ya thamani ya mzigo (FOB Value) kwa nyama zinazouzwa nje ya nchi.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki alisema hayo jana, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Wizara imeliomba Bunge kuwaidhinishia Sh169.19 bilioni ambapo kati ya hizo, Sh47.84 bilioni ni kwa ajili ya sekta ya mifugo, huku Sh121.35 bilioni zikiwa ni za sekta ya uvuvi.

Ndaki alisema wizara imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa wadau wa sekta ya mifugo kuhusu ada na tozo mbalimbali, hususan tozo ya asilimia moja ya thamani ya mzigo (FOB Value) kwa nyama zinazouzwa nje ya nchi na ada ya ukaguzi wa mazao ya mifugo.

"Kutokana na hali hiyo, wizara imefanya mapitio ya tozo hizo ili kuzibadilisha, lengo likiwa ni kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na kuongeza mauzo ya mazao ya mifugo nje ya nchi," alisema. Alisema maboresho yaliyofanyika yatawasilishwa na waziri wa fedha na mipango wakati akiwasilisha muswada wa sheria ya fedha (Finance Bill) ya mwaka 2021/2022.

Alisema katika mwaka 2021/2022, wizara yake itaendelea kutathmini tozo na ada mbalimbali zitakazoonekana kuwa kero kwa wazalishaji na wafanyabiashara wa mifugo na mazao yake, ili kuzifuta au kuzifanyia marekebisho.

Kuhusu kodi katika sekta ya uvuvi, Ndaki alisema Serikali imepunguza viwango vya tozo na ada mbalimbali katika uzalishaji na usafirishaji wa mazao ya uvuvi nje ya nchi.

Alisema punguzo hilo lilitangazwa katika gazeti la Serikali la Juni 29 mwaka huu iliyoanza kutumika Julai 2020, lengo likiwa ni kupunguza gharama na kuhimili ushindani wa kibiashara ndani na nje ya nchi. Alitaja baadhi ya viwango vya tozo ya usafirishaji wa dagaa nje ya nchi kutoka Ziwa Tanganyika ambayo imepungua kutoka Dola za Marekani 1.5 hadi Dola za Marekani 0.5 kwa kilo.



**"...tozo nyingine ni ya usafirishaji wa samaki aina ya migebuka kwenda nje ya nchi imepungua kutoka Dola za Marekani 0.5 hadi Dola za Marekani 0.3 kwa kilo."**

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki

Nyingine ni usafirishaji wa dagaa nje ya nchi kwa dagaa wa bahari, Ziwa Nyasa na Ziwa Victoria kutoka Dola za Marekani 1 hadi Dola za Marekani 0.16 na ada ya leseni ya kusafirisha dagaa nje ya nchi kwa wafanyabiashara wadogo imepungua kutoka Dola za Marekani 1,000 hadi Dola za Marekani 250 na kwa wafanyabiashara wakubwa kutoka Dola za Marekani 1,800 hadi Dola za Marekani 500.

Tozo nyingine iliyopungua ni ada ya leseni ya mazao mengine ya bahari kama pweza, kambakochi na kaa imepungua kutoka Dola za Marekani 2,500 hadi Dola za Marekani 500 kwa wafanyabiashara wadogo na kutoka Dola za Marekani 2,700 hadi Dola za Marekani 1,000 kwa wafanyabiashara wakubwa.

**Meli nne kubwa za uvuvi**

Ndaki alisema kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (AFDP) imepata mkopo wenye masharti nafuu kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo (IFAD) kwa ajili ya kununua meli nane za kuvua katika ukanda wa uchumi wa Bahari Kuu.

Alisema kati ya meli hizo, nne zitakuwa Tanzania Bara chini ya Kampuni ya Uvuvi Nchini (Tafico) na nne nyingine Zanzibar chini ya Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (Zafico). Alisema kwa upande wa Tanzania Bara, meli mbili za mwanzo zitanunuliwa mwaka 2021/2022 na meli nyingine mbili mwaka 2023/2024.

**Bei elekezi uogeshaji mifugo**

Ndaki alisema wizara imefanya mapitio na kuboresha kanuni na mwongozo wa uogeshaji ambao unatoa maelezo ya namna ya uogeshaji mifugo.

"Kanuni na mwongozo huo umeainisha majukumu ya wadau ikiwemo bei elekezi ya kuogesha mifugo ya Sh50 kwa ng'ombe na Sh10 kwa mbuzi au kondoo," alisema. Kuhusu homa ya nguruwe, waziri huyo alisema ugonjwa huo ulioripuka kwa vipindi mbalimbali katika mwaka 2020/2021 ulisababisha vifo 5,428 katika halmashauri 18 Tanzania Bara.

Alisema ugonjwa huu hauna tiba wala chanjo, hivyo alitoa wito kwa halmashauri zitoe elimu ya namna ya kujikinga na ugonjwa.

Scanned with CamScanner